Barua pepe:lajijidodoma5@gmail.com
Ijumaa Machi 5 - 2021



# HABARI ZA DODOMA



*Diwani wa Kata ya Mnadani, jiji la Dodoma, Paul Bankiye akizungumza na wakazi wa Mtaa wa Mbwanga kwenye mkutano alipokuwa akitoa ufafanuzi kuhusu kero za upimaji wa ardhi na kulasimisha makazi yao uliofanyika jana. Picha na Lucas Peter*

# Profesa Ole Gabriel aitaka LITA kuzalisha wataalam itakaowaajiri

■ Na Omary Mtamike, WMU

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel, ameitaka Wakala ya Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo nchini (LITA), kuzingatia maadili na uadilifu wakati wa utekelezaji wa majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanatenda haki ndani na nje ya taasisi hiyo.

Prof. Ole Gabriel alisema hayo jijini Dodoma wakati akifungua mkutano wa baraza la nane la wafanyakazi wa taasisi hiyo na kupongeza utaratibu wa kukutana mara kwa mara kwa baraza hilo na kusisitiza mikutano ya namna hiyo inapaswa iwe na tija kwa watumishi na wanufaika.

"Mkutano huu ni mkubwa sana na una heshima yake, hivyo ni vizuri utumike kujadili kwa kina namna ya kupunguza na kuondoa changamoto za watumishi wa kampasi zote za LITA ili ziweze kutekeleza vyema jukumu la kuzalisha wataalam wa tasnia ya ufugaji hapa nchini," alisisitiza Prof. Ole Gabriel.

Aidha, Prof. Ole Gabriel alitoa wito kwa kampasi zote za taasisi hiyo kuhakikisha zinabadilisha mifumo yake ya ufundishaji ili kuwafanya wahitimu wa vyuo hivyo kuweza kujiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa kama ilivyozoeleka kwa sasa.

"Huwa inanisikitisha sana kumuona mzazi anamgharamia mwanae karo ya masomo kwa miaka isiyopungua mitatu, halafu baadaye mzazi huyo anaanza kuwajibika kumtafutia mtoto wake ajira.

"Lazima tubadilishe huu mtazamo kwa sababu chuo chenu kimejikita zaidi kwa vitendo…zalisheni wataalam watakaojitegemea kwenye soko la ajira," aliongeza.

Prof. Ole Gabriel alitaka LITA kuhakikisha inazingatia usawa wa kijinsia katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ndani ya taasisi hiyo ikiwa ni pamoja na kuwapa nafasi wanawake katika ngazi mbalimbali wanazostahili.

"Kuwa mnene au mwembamba ni juhudi za mtu binafsi lakini kuwa mwanamke au mwanaume ni uamuzi wa Mungu, hivyo si vyema kushindwa kumpa mtu nafasi kisa ni mwanamke na kufanya hivyo kwa kweli ni kosa kubwa sana," alisema.

Awali akitoa taarifa ya utangulizi kuhusu mafanikio ya LITA, Mtendaji Mkuu wa taasisi hiyo Dkt. Pius Mwambene alisema katika kipindi cha mwaka uliopita taasisi hiyo imefanikiwa kuongeza nafasi ya udahili wa wanafunzi kutoka 2,536 hadi wanafunzi 3,574 mwaka huu.

"Hata hivyo kutokana na ongezeko hilo, tumekuwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na mabweni, madarasa, maabara, maktaba na walimu wa fani za afya ya mifugo na uhandisi kilimo ambapo mpaka sasa tunahitaji walimu 34," alisema Dkt. Mwambene.

AidhaDkt. Mwambene alibainisha juu ya uwepo wa changamoto ya uchakavu wa miundombinu ya taasisi hiyo ikiwa ni pamoja na majengo ambayo kwa sehemu kubwa yanatakiwa kuvunjwa na kujengwa mengine.

"Katibu Mkuu, fedha za kuendesha shughuli mbalimbali za vyuo tutapambana tujihudumie wenyewe ila tunaomba wizara itusaidie tupate fedha za maendeleo kwa ajili ya kujenga miundombinu hii kwa sababu imeshakuwa ya muda mrefu mno, yapo majengo yana zaidi ya miaka 80," aliongeza.

Scanned with CamScanner

Ntinika alitoa amri hiyo jana, wakati wa mkutano mkuu wa

hatuwezi kuwaacha hivi hivi wa-

vya ushirika vikiwamo vya akiba

# Wanufaika TASAF washauriwa kufanya ufugaji

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune, amezitaka kaya zote zinazowezeshwa na Mpango Taifa wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF), kujishughulisha na ufugaji wa kuku pamoja na bata wa asili kwa madai kuwa mifugo hiyo inastahimili magonjwa, lakini soko lake ni la uhakika.

Alitoa ushauri huo jana wakati wa ziara ya kuzitembelea kaya zinazonufaika na TASAF zilizopo Kijiji cha Mpakani, Kata ya Ubaruku, kusikiliza vikwazo vinavyowakabili na kuangalia shughuli wanazozifanya baada ya kunufaika na mfuko huo.

Alisema ufugaji wa bata wa asili na kuku ni miongoni mwa mifugo ambayo hutumia gharama kidogo kuendesha ikilinganishwa na mifugo mingine na kushauri kufuga mifugo hiyo ili kupata faida na kumudu gharama za maisha.

"Serikali itaendelea kuwawezesha wananchi kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini TASAF, kwa kuwapa mitaji elimu ya ujasiriamali na masuala mengine kwa ustawi wa uchumi wao, naamini wengi wao wameongeza kwa kufungua miradi ya kujiingizia pesa, nawahamasisha endeleeni kujifunza na kutafuta shughuli nyingine," alisema Mfune.

Kuhusu usimamizi na namna ya kuhudumia mifugo hiyo, alisema atawaagiza maofisa ugani kuwatembelea mara kwa mara ili kuwapa elimu ya utunzaji na kuepukana na magonjwa ikiwamo kuwahudumia vizuri na kupata soko la uhakika.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mpakani, Amos Mgongolwa alisema kwa mara amekuwa akimara kwa mara amekuwa akiwatembelea wananchi wake kwa lengo la kuangalia shughuli za maendeleo wanazozifanya ikiwamo ujasiriamali.

Alimshukuru Mkuu wa Wilaya kwa kuwatembelea wananchi wa eneo hilo na kuwapa mbinu ya ufugaji wa bata wa asili pamoja na bata ili kujiongezea kipato kupitia uwezeshwaji wa TASAF.

Miongoni mwa wanufaika wa TASAF, Bupe Mwaisumo alisema fedha za mfuko huo zimemuwezesha kufungua biashara yake ambayo kwa sasa inamsaidia kuendesha maisha yake ikiwamo kusomesha, chakula na malazi.

Alisema ana unafuu wa maisha ikilinganishwa na ilivyokuwa awali kwa kuwa licha ya majukumu ya kuendesha familia, anaweza kupata akiba na kufanya masuala mengine ya maendeleo.

Scanned with CamScanner

# Serikali, FAO wajipanga kuboresha uvuvi Ziwa Tanganyika

Na Jasmine Shamwepu

SEKTA uvuvi inachangia asilimia 1.7 katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Hata hivyo, licha ya asilimia kubwa ya nchi yetu kuwa na sehemu kubwa iliyozungukwa na maziwa, mito na bahari, lakini mchango wa sekta ya uvuvi bado haujaleta mafanikio ya kutosha ...

[illegible]



Wachuuzi wa samaki na dagaa wanaonunua kwenye Ziwa Tanganyika ni miongoni mwa wadau watakaonufaika na maboresho ya uvuvi, ambayo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Shirika la Chakula na Kilimo (FAO) wameratibu.

[illegible]

### KODI KWA WAFANYABIASHARA

[illegible]

### ZANA DUNI

[illegible]

### MTAMBO WA BARAFU

[illegible]

### FAO WANACHOSEMA

[illegible]

### UCHUNGUZI

[illegible]

### TAASISI YA TAFITI

[illegible]

# 'Samaki wanaokufa Ziwa Victoria hawana sumu'

Na Vicky Kimaro

SERIKALI imesema samaki wanaokufa katika Ziwa Victoria hawana sumu, lakini haishauri watu wawatumie kwa kitoweo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk Rashid Tamatama, aliyasema hayo juzi na kueleza kuwa, baada ya uchunguzi wa sampuli walizopeleka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali, majibu yameonesha samaki hao hawana sumu.

Mwezi mmoja uliopita, samaki aina ya sangara wanaoweza kukua na kufikia zaidi ya kilogramu 100 walionekana wakielea majini wakiwa wamekufa katika ziwa hilo maeneo ya Kenya na Uganda.

Dk Tamatama alisema wiki moja baada ya samaki hao kuonekana wamekufa, walifanya uchunguzi kuanzia Rorya hadi Bukoba.

"Kwa takribani wiki mbili sasa, maeneo ya Rorya na Bukoba samaki wengi wameonekana wakiwa wamekufa sababu ilikuwa haijulikani, hali hiyo ilianza kutokea mwezi mmoja uliopita katika maeneo ya Kenya na Uganda," alisema.

Alisema walichukua sampuli katika maeneo ya Musoma, Nyamikoma, Sengerema, Geita, Bukoba na kuzipeleka kwa mkemia mkuu ili kuangalia kama zina sumu au walikufa kifo cha kawaida.

"Matokeo yanaonesha hakuna samaki yoyote aliyekutwa na sumu, inathibitisha alichoongea Dk Ishmael Kimerei kuwa wamekufa kwa kukosa hewa kwa sababu kwenye Ziwa Victoria yale maji huwa muda wote kuna leya ya maji ya chini hayachanganyiki na leya ya maji ya juu," alisema.

Dk Tamatama alisema katika ziwa hilo maji ya chini joto lake lipo chini na ya juu mara nyingi joto ni la juu.

"Ziwa Victoria kuanzia mita 20 oksijeni huwa haipo, kwa muda mrefu hayo maji yanakaa hivyo leya mbili hazichanganyiki, sasa kuna muda hali ya tabianchi ziwani maji yanachanganyika ya juu yanaenda chini na ya chini yanaenda juu hasa miezi ya baridi na kipupwe," alisema.

Kwa mujibu wa Dk Tamatama, maji ya chini ni mengi kuliko ya juu na yakipanda juu yanakuwa hayana oksijeni hivyo kuwaathiri samaki na kwamba, wanaoathirika zaidi ni samaki wakubwa kama sangara.

Scanned with CamScanner

# Malalamiko ya wavuvi kufanyiwa kazi

Na Vicky Kimaro

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, amemtaka Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk Rashid Tamatama kuhakikisha anakamilisha utafiti wa malalamiko ya kanuni ya mwaka 2020 ambao umekuwa ukifanywa na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania(TAFIRI) kabla ya Machi 23.

Akizungumza Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Paulina Gekul alisema kanuni hizo za mwaka 2020 zimekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wavuvi kuhusu mita 50 za bahari, uvuvi wa nyavu mtando na kutaka kazi hiyo ikamilike haraka kabla ya Machi 23.

Gekul alimtaka katibu mkuu huyo kuhakikisha wavuvi wote ambao hawajashirikishwa wanashirikishwa ipasavyo.

Alieleza kuwa changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa marekebisho ya kanuni za uvuvi za mwaka 2020 serikali imeazimia kuzipitia upya ili ziendane na mahitaji ya sasa.

Alisema hivi karibuni wizara imepokea maoni na changamoto mbalimbali kutoka kwa wadau wa sekta ya uvuvi kutoka Ukanda wa Bahari, Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria kuhusiana na marekebisho ya kanuni ya uvuvi ya mwaka 2020 katika baadhi ya vipengele.

Gekul alisema maeneo ambayo yameonesha kuwa na changamoto nyingi ni katika uvuvi wa kutumia nyavu za mtando wakati wa mchana katika ukanda wa Bahari ya Hindi, utaratibu wa kupima ukubwa wa macho ya nyavu kwa kutumia kipimo kilichoainishwa katika kanuni kinachofahamika kama Mesh Gauge na uvuvi wa dagaa wakati wa mbalamwezi.

Kutokana na changamoto hizo, Waziri wa Mifugo, Mashimba Ndaki hivi karibuni alitoa maelekezo kuwa TAFIRI ifanye utafiti kuhusu uvuvi wa kutumia nyavu za mtando na hivyo inatakiwa kutoa majibu kabla ya Machi 23.

Aidha Gekul alisema wizara haifurahishwi sana kuwa na msururu wa makatibu wakuu wa vyama vya wavuvi.

"Kuna katibu Mkuu Uvuvi, Dar es Salaam, Katibu Mkuu Uvuvi ziwa Victoria, Katibu Mkuu Ziwa Tanganyika, Katibu Mkuu kila mahali, nakuagiza Kaitbu mkuu wa wizara yetu Tamatama lisimamie hili haraka sana kuhakikisha mnawaunganisha wote na kuwa na chama kimoja.

Scanned with CamScanner

# Serikali: Samaki Ziwa Victoria hawakufa kwa sumu

**Dar es Salaam.** Serikali imewaondoa hofu wananchi kuhusu samaki aina ya sangara waliokutwa wamekufa maeneo mbalimbali ya Ziwa Victoria, ikiwamo Bukoba na Rorya ikisema hawakufa kwa sumu bali ni vifo vya asili.

Kauli hiyo ilitolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Uvuvi, Dk Rashid Tamatama wakati wa majumuisho ya mkutano wa siku tatu wa wadau wa sekta ya uvuvi, uliofanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali, akiwamo Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda.

**(Bakari Kiango)**

Scanned with CamScanner

ers from the area could prove difficult as herders use arrows to protect themselves.

**Omar Sayid (L), an engineer with Tanga-based Oxygen Product East Africa Ltd, briefs journalists yesterday on the use of nitrogen in industrial operations. Right is the firm's owner, Mohammed Sayid. Photo: Correspondent Boniface Gideon**

# 'LITA weighed down by shortage of tutors, rundown infrastructure'

**By Guardian Reporter**

LIVESTOCK Training Agency (LITA) chief executive officer Dr Pius Mwambene has said last year the institution was able to increase students' enrolment from 2,536 to 3,574 this year.

He said due to the increase, LITA has been faced with various challenges, including insufficient students' accommodation, lecture halls, laboratories, libraries and teachers in the livestock health, and as for now there is shortage of 34 teachers.

He also cited the challenge regarding dilapidated infrastructures in the institution including many buildings which need to be demolished and replaced by new buildings.

Dr Mwambene's remarks were given in his introduction speech at the opening of the opening the 8th LITA Workers Council which was officially opened by the Livestock and Fisheries Permanent Secretary Prof Elisante ole Gabriel.

Prof Gabriel praised the tendency of meeting regularly, stressing that such meetings should be beneficial to all workers.

He also called on LITA to adhere to ethics and trust in implementing its duties to ensure it acts justly within and outside the institution.

"This is a huge meeting and it carries its own respect hence it is better for it to be used to discuss in-depth on how to reduce or eliminate changes of all workers of LITA's campuses to enable it to produce qualified experts for the country's livestock sector," said Prof Gabriel.

He also called upon all campuses to ensure they change their teaching systems to ensure graduates become self-employed instead of waiting to be employed as it is now.

He required LITA to ensure it abides by gender equality in its implementation of its various responsibilities, including giving women positions in levels they deserve.

Scanned with CamScanner